1013/1

MTHANI WA MWIGO -2019

KISWAHILI

KARATASI 1

MUDA: SAA 2

MAAGIZO.

1. Mtihani huu una sehemu nne; Insha, Ufahamu, Matumizi ya lugha na Sajili ya lugha Ni muhimu ufuate maagizo yote uliyopewa.
2. Andika majibu yote katika sehemu ulizoachiwa.

| **SEHEMU** | **SWALI** | **UPEO** | **ALAMA** |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 20 | |
| 2 | 2 | 20 | |
| 3 | 3 | 50 | |
| 4 | 4 | 10 | |
| | | **JUMLA** | |

SEHEMU YA KWANZA (ALAMA 20)

INSHA: Andika insha isiyopungua kurasa mbili juu ya mojawapo wa mada zifuatazo.

1. Andika mahojiano baina ya mwanahabari ( Mwandishi wa Taifa Leo) akimhoji mbunge kuhusu mpango wa miradi ya hazina ya eneo – bunge analowakilisha.
2. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo:

   Sasa lilikuwa zogo si zogo, vilio si vilio…………………..
3. Wanawake ni kigezo muhimu katika kufanikisha maendeleo nchini. Jadili
4. Ivushayo ni mbovu.

1. SEHEMU YA PILI - UFAHAMU - (ALAMA 20)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali

Mzee Bakuli alianza kuwa mlevi wa kupindukia na mwisho akafilisika sana na hata alishindwa kuubeba mzigo wake wa nyumba. Shinda zikawa zinazidiana kila leo. Mkewe kwa <u>kutaka</u>

kujenga nyumba isibomoke alijaribu kumwonya mumewe juu ya ulevi lakini hakuambulia lolote. Mwisho aliona ni vema kumpeleka mumewe kwa balozi ili akasemwe na wazee lakini hata huko aliambulia nunge. Mzee bakuli hakuona kuwa hiyo ilikuwa ni dawa. Maneno yaliingilia huku yakatokea kule na hakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Ndio kwanza alizidi kukaza kamba! Kila mtu alibaki kumtazama tu.

Siku moja katika pilikapilika zake mitaani alikutana na rafiki yake aliyejulikana kwa jina Samahani. Watu hawa walishibana vilivyo. Baada ya salamu na maongezi ya mkato, waliona ni heri wapitie kilabuni kuonja. Hapo kilabuni onjaonja ilivuka mipaka, wakaona tu saa zinapita. Walipiga mtindi wa mwaka. Ilipopata saa sita za usiku wakaona tu hawajiwezi, wakashauriana kwenda makwao. Hapakuwa na aliyeweza kumsindikiza mwenzake kwani wote walikuwa ndi! Mzee Bakuli alijikokota lakini mwishowe aligota kwani nguvu zilimuishia, akashikwa na usingizi wa pono. Bila ya kujichagulia pahali pazuri pa kulala, alijibwaga chini akalala karibu na barabara kama mfu, mdomo wazi na macho aliyafumba nusu. Baada ya saa mbili kupita alionekana na wapiti njia wahuni ambao walipapasapapasa mifuko yake na kumchukulia akiba yake yote, Kisha wakajifanya wasamaria wema wakaelekea katika kituo cha polisi na kuwaeleza kuwa wamemuona mtu aliyekufa.

Muda si muda polisi alileta gari na bila kumpima kinyume cha kawaida yao walimpeleka hospitali ili akawekwe katika chumba cha maiti. Ajabu daktari aliposikia kuwa ni kimba, naye kinyume cha wajibu wake, hakuona haja ya kushughulikia kitu kilichokwisha kazi. Kwanza, kifo kilikuwa kimethibitishwa. Kwa hivyo akajifanya kuwa anampimampima kasha muda si muda akaamuru apelekwe kwenye chumba cha maiti nayo amri ikatimizwa.

Shuhudia basi yaliyotokea! Maajabu yalikuwa si maajabu! Ilipotimu saa kumi na moja ya asubuhi, mlevi aliamka, akili zikaanza kumjia pole-pole akadhani yuko nyumbani mwake. Akaanza kujinyoosha, mara zikagutuka na katanabahi ya kwamba alikuwa katika makao ya wafu. Akili zikamduru kwanza akadhani anaota lakini mwisho aling'amua kuwa ni mambo ya kweli. Hapo alipiga mayowe na kugonga mlango kwa fujo. Mlinzi wa chumba cha maiti alipata mshangao na kuogopa sana akifikiria kwamba huenda kiama kimekuja.

Vipi mtu tena kufufuka! Huku akitetemeka aliufungua mlango na kwa ghafla aligutushwa zaidi na mshindo wa mtu aliyetoka mithili ya risasi, akikimbilia sehemu za mashambani. Huyo hakuwa mwingine bali alikuwa ni Mzee Bakuli. Mlinzi naye alipiga mbio bila kujua alipokuwa akielekea kwa kuogopa kuwa huenda akatokea mwingine na hata kama ilikuwa ni siku ya ufufuo hakupenda imfikie katika chumba cha maiti. Alipofika kwake aliamua mambo heri yawe yatakavyokuwa nayo, ilimtoa roho kiasi hicho. Na huo ukawa mwisho wa kazi yake katika chumba cha maiti.

Bakuli aliendelea na mbio zake kwa madhumuni ya kufika kwake kabla ya kupambazuka. Alipishana na vijinyama vya mwituni bila kuvuja na kuviacha na mshangao. Punde si punde Bakuli aliingia kwake kwa hodi ya mshituo. Mkewe alipomfungulia mlango alitahamaki mno kwa kumuona mumewe katika hali mbaya, akatambua kuwa mambo hayakuwa mazuri. Alimshugulikia vilivyo na kumfichia aibu.

Mzee Bakuli alipotulizwa alieleza kisa chake akapewa pole na mkewe. Alipoulizwa kama atarudia ulevi tena alisema hataki tena habari za pombe hatataka urafiki na walevi kwani mtupa jongoo hutupa na mti wak.Alijuta kwa kujiaziri nakuridisha maelendeleo ya watu wake nyuma kwa muda wote huo. Kulipokucha alitaka balozi aitwe pamoja na wazee wa kitongoji chao.

Wazee wote walipobarizi aliwaomba msamaha na wakaishi kwa raha mstarehe. Bakuli alibadilika na kuwa ‘ mtu’. Hakugusa pombe tena na baada ya miaka miwili walifanya mambo mengi sana ya maana.

MASWALI.

a. Mzee Bakuli alikuwa na tabia gani? (al. 2)

b. Mke wa Bakuli alikuwa ameonyesha mwenendo gani katika kuupenda unyumba? (al.2)

c. Kinyume na sifa zao askari na daktari wanaweza kulaumiwa vipi?(ala. 2)

d. Katika habari hii mwandishi amejitokeza kama mtumiaji wa vichekesho. Taja mifano mitatu ya vichekesho hivyo. (al.3)

e) Andika methali inayodhihirishwa bayana na ujumbe unaopatikana katika kifungu hiki?

(al 2)

f) Mlinzi wa chumba cha kuhifadhia maiti alichukua hatua gani baada ya kisa kilichompata? (al 2)

g) Mzee Bakuli aliamua kutupa jongoo na mti wake. Ina maana gani? Al 2.

h) Eleza mafungu yafuatayo ya lugha kama yalivyotumiwa katika kifungu.( al 4.

i) Kutaka kujenga nyumba isibomoke.

ii) Ndio kwanza alizidi kutaka kamba

iii) Katanabahi

iv) Kimba

2. SCHEMU YA TATU.

MATUMIZI YA LUGHA.

Jibu maswali yote katika nafasi ulizopewa (alama 50)

1. Andika Kwa wingi. (al. 2)

Wembe uliomkata ulikuwa na kutu.

2. Andika kwa uyakinifu (al.2)

Wasingalikuwa wajanja wasingalipatikana.

3. Andika kinyume (al.2)

Mama aliezeka nyumba hii

4. Weka nomino hizi katika ngeli zake. (al 2)

Kibogoyo ____________________________________________________________

Kibofu ____________________________________________________________

5. Unda sentensi itakayoonyesha (al 2)

N+ V+ T+ N

6. Andika kwa ukubwa ( al 4)

(i) Nyumba hii ilinunuliwa na mzee yule

(ii) Kijoka kilikiuma kijiguu.

7. Andika kwa usemi halisi (al2)

Maria alitaka kujua kama wangeenda mchezoni siku iliyofuata.

8. Changanua kwa njia ya jedwali (al 4)

Mwanafunzi huyu atachelewa leo

9. Tunga sentensi kwa kutumia neno <u>kwa</u> kuonyesha kusudi au nia (al.2)
10. Andika katika hali ya mazoea (al2)
    Mtoto aliyelia alichapwa.
11. Akifisha (al.2)
    Ali utaenda nairobi leo.
12. Nyambua neno lililo kwenye mabano katika kauli ya kutendeka. (al. 2)
    Karimi ame(maliza) masomo yake (al 2)

13. Unda nomino nyingine kutokana na ile umepewa (al.2)
    i) Mwalimu
    ii) Msafiri

14) Mapambo haya huvaliwa wapi? (al.2)
    Kipini ________________________________________________
    Njuga ________________________________________________

15) Haya ni malipo gani?
    Mahari ________________________________________________
    Fungule ________________________________________________

16) Kigari kidogo kinachosukumwa kwa mikono kinachotumiwa kubebea mizigo huitwa (al2)

17) Andika kwa maneno ( al 2)
    1,000,505
    ii) 5/8

18. Ugonjwa wa kuharisha na kutapika huitwa ______________________________ (al2)

19. Dada ya mama huitwa __________________________ dada ya baba huitwa ______________ ( al 2)

20. Ndege mwenye shingo ndefu na miguu mirefu huitwa __________________________ (al 2)

21. Sehemu ya mwili inayasawazisha sukari mwilini huitwa _______________________ ( al2)

22. Mtu anayekubali kutumiwa | Kutumikia mwingine ili kupata manufaa ya kibinafsi huitwa _______________________ ( al2)

23. Tunga sentensi moja kubainisha maana ya maneno haya ( al 2)

Apa

Hapa

SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (AL10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Mhusika 1: Mia! One hundred! Mia! One hundred! Bei rahisi.
Jibebee mali sasa! Ni ya leo, ni ya leo.

Mhusika 2. Shika mia hii.

a) Hii ni aina gani ya sajili? ( al 1)

b) Mhusika wa 1 na wa 2 ni akina nani? (al 2)

c) Taja sifa za sajili hii (al 7)